CATHOLIC SECRETARIAT

TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE

P.O BOX 2133
PHONE 022/2851075-7-8
022/2850047
022/2850017
FAX 022/2851133; 2850427
DOMAIN: TEC.CO.TZ
E-Mail: info@tec.or.tz
DAR ES SALAAM
TANZANIA
01-01-2026

***Department:*** **LITURGY**

***Reference:*** ***TEC/Lit/Music 010126***

Mratibu wa UKWAKATA Taifa
Waratibu wa Liturujia Majimbo yote
Viongozi UKWAKATA Ngazi zote.

**Tumwimbie Bwana**

**YAH: MAREKEBISHO YA MUZIKI AWAMU YA PILI: MISA SITA**

Wapendwa katika Kristo,

Kamati ya Muziki Mtakatifu Taifa, imekamilisha marekebisho ya Misa nyingine sita kati ya ishirini zilizopendekezwa kuwa yaingizwe maneno sahihi kadiri ya tafsiri ya Misale ya Kiroma toleo la sasa. Hizi ni kati ya tungo za Misa ambazo pasipo mashaka kwa miaka mingi zimekuwa zinaimbwa sana katika maadhimisho ya Liturujia ndani na nje ya Tanzania. Marekebisho haya yanatupa jumla ya misa 13 zilizokamilika.

Misa zilizokamilika kwa awamu hii ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Misa ya XI (Felician Nyundo) | 4 | Misa ya Shauritanga (Antony J Haule) |
| 2 | Misa ya XII (Felician Nyundo) | 5 | Misa ya Wafu (Gregory F. Kayetta) |
| 3 | Misa ya Shukrani (Joseph Makoye) | 6 | Misa ya Mt. Yakobo Na. II (Gregory Kayetta) |

Lengo la marekebisho ni mwendelezo wa kuondoa ombwe lililotokea baada ya kupata tafsiri mpya ya Misale ya Kiroma na kuendeleza umoja wa uimbaji katika Kanisa la Tanzania.

Kwa kuwa watunzi wa Misa hizi wengi wamepumzika katika makao ya milele, Kamati ya Muziki Mtakatifu-Taifa imepewa dhamana ya kufanya marekebisho kwa manufaa ya Kanisa zima. Kamati imezingatia marekebisho ya maneno kwa kuiga umbo na mwafaka wa kimuziki bila kuathiri mno kazi ya mtunzi wa Misa hiyo; isipokuwa pale ilipolazimu. Kamati imejitahidi sana kuepuka kufanya utunzi mpya.

Kwa barua hii Idara ya Liturujia-TEC, inapokea na kuyapa ithibati marekebisho hayo, na inasitisha rasmi matumizi ya toleo lolote la nyuma na kuidhinisha matumizi ya toleo hili kama lilivyo wasilishwa na Kamati ya Muziki Taifa.

Tungo hizi za Misa sasa zinapatikana katika tovuti yetu **https:wwwk.swahilimusicnotes.com/** (SMN) katika kundi la MISA-TEC.

Kwa maombezi ya Bikira Maria Mama wa Mungu, tunawaombea wana-UKWAKATA ili mziimbe nyimbo hizi katika kumtukuza Mungu na Wanakanisa wajipatie utakatifu.

**Wenu katika Utumishi**

TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE
LITURGICAL DEPARTMENT
P. O. BOX 2133,
DAR ES SALAAM-TANZANIA

Jandu.

..........................................................

Pd. Clement Kihiyo
Katibu Mtendaji-Idara ya Liturujia-TEC